**HAI RURAL TEACHERS SAVINGS AND CREDIT CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED**
**P. O. BOX 8 HAI-KILIMANJARO**
**PHONE: +255 27 275 0208/+255 715 371153,**
**www.hrtsaccos.org**
**Email: info@hrtsaccos.org.**
**REG: PRI-KJR-HAI-DC-2022-1418**
**LESENI DARAJA B, MPS3-TCDC-2023-00328**

# MKATABA WA MKOPO

Mkataba huu umefanyika leo hii siku ya ………… ya mwezi………..mwaka 20…......... Baina ya Chama cha Akiba na Mikopo cha HAI RURAL TEACHERS SACCOS chenye namba ya usajili KLR 547 kilichoanzishwa kwa mujibu wa sheria ya vyama vya Ushirika Namba 6 ya Mwaka 2013,( na Kanuni zake) na anwani yake ni S.L.P 8 HAI (ambacho katika Mkataba huu kitajulikana kama MKOPESHAJI) kwa upande mmoja.

**Na**

Ndugu ………………………………………………………………….. ambaye ni Mwanachama wa Chama mwenye check no. ………………………….. wa S.L.P….…………………….........na mwenye namba ya simu……………………………..(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **MKOPAJI** na neno "Mkopaji" linaweza kujumuisha Warithi wa mali za Mkopaji, wamiliki, wasimamizi au wadhamini wake, kadri itakavyohitajika), kwa upande mwingine.

**KWA KUWA:**

(i) **MKOPESHAJI** baada ya kuzingatia maombi yaliyowasilishwa na **MKOPAJI** amekubali kumpatia huduma ya mkopo **MKOPAJI** kwa mujibu wa Masharti na Sera ya Mikopo ya Chama.

(ii) **MKOPAJI** ameomba kwa hiari yake kupatiwa huduma ya mkopo kutoka kwa **MKOPESHAJI.**

**KWA HIYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA KWAMBA:-**

1. Baada ya kutiwa saini kwa mkataba huu, Mkopeshaji atampatia Mkopaji mkopo wenye thamani ya fedha za kitanzania za Tshs……………………………. [TAJA KIASI KWA TARAKIMU] …………………………........................................................................... [TAJA KIASI KWA MANENO] na Mkopaji anakiri kupokea kiasi kilichotajwa.
2. Mkopaji anaahidi kuwa atarejesha mkopo aliochukua na riba ya asilimia ……………..…….. kwa mwezi

3. Muda wa marejesho ya mkopo ni miezi ………………… na kwa maana hii mkopaji atarejesha mkopo huo kikamilifu pamoja na riba yote.
4. Ninakubali kukatwa kwenye mshahara wangu kupitia mwajiri wangu kiasi cha marejesho ya mkopo pamoja na riba Tshs……………………………………kila mwezi kwa madhumuni ya kutimiza masharti ya ulipaji mzuri wa mkopo niliochukua HRT SACCOS hadi deni litakapomalizika kuendana na makubaliano ya muda wa marejesho.
5. Ninamuidhinisha mwajiri wangu itokeapo kukoma kwa ajira yangu iwe kwa kuacha kwa hiari, kufukuzwa, kupunguzwa au kustaafu kulipa HRT SACCOS mafao yangu kama malipo ya salio la mkopo.
6. Naahidi kulipa mkopo wangu kwa fedha taslimu ofisini kila mwezi kama itabainika kuna tatizo au makato hayajafanyika kwa wakati toka kwenye mshahara wangu
7. Endapo nitachelewesha marejesho ya mkopo kuendana na masharti ya chama nitalipa adhabu stahilki ya 10% ya rejesho la kila mwezi.
8. Iwapo nitakatisha Mkataba nalazimika kulipa mkopo wote pamoja na riba iliyokadiriwa na chama na nitakapohitaji kusitisha uanachama nitalipa mkopo pamoja na riba ninayodaiwa.
9. Iwapo mkopo wangu utanunuliwa na taasisi nyingine yeyote ya fedha nitawajibika kulipa asilimia 5 ya deni langu lililonunuliwa.
10. Mkopaji ameweka mali zilizotajwa hapa chini kama dhamana ya mkopo ambazo ni pamoja na Hisa za hiari, Akiba, Akiba ya dharura na dhamana za wadhamini.
    i. Hisa za hiari zenye thamani ya shilingi ………………………………………
    ii. Akiba yenye thamani ya shilingi……… ……………………………………….
    iii. Akiba ya dharura yenye thamani ya shilingi ………………………………
    iv. Mali ya Mkopaji na eneo iliyopo…………………………………………………………
    v. Amana ya muda maalum (fixed deposit)…………………………………………….
    vi. Mali za Wadhamini ………………………………………..……..zenye thamani ya Tshs……………………..……. zilizopo…………………………………………………
11. Nakubali kukatwa asilimia 1 ya mkopo kwa ajili ya mfuko wa majanga (kama mkopo unaanzia Tshs 1,500,001) ili kufidia deni langu itakapotokea kifo au ulemavu wa kudumu utakaothibitishwa na daktari ndani ya muda wa mkataba.
12. Kwa mujibu wa mkataba huu, mkopaji, mdhamini/wadhamini wa mkopaji hawataruhusiwa kuhamisha umiliki, kuuza, kupunguza au kutumia kama dhamana, mali iliyowekwa dhamana hadi deni lote pamoja na riba litakapokuwa limelipwa.
13. Mkopaji akishindwa kulipa deni lote na riba au kimoja wapo katika muda uliopangwa, Mkopeshaji atakuwa na haki ya kuchukua hatua za kisheria kukomboa deni lake ikiwa ni pamoja na kutwaa na kumiliki dhamana

iliyowekwa au kuuza dhamana hiyo ili kulipa deni bila kulazimika kuomba mamlaka ya kisheria ya kufanya hivyo, baada ya kumtaarifu kwa Maandishi Mkopaji.

14. Iwapo mkopaji atashindwa kulipa deni lote na riba au kimojawapo na mkopeshaji akaamua kuchukua hatua za kisheria kama ilivyokubaliwa hapo juu ikiwa ni pamoja na kutwaa mali ya dhamana, kuuza au kufungua shauri ili kudai au kufidia deni gharama zote za kutekeleza hatua hizo zitalipwa na mkopaji.
15. Kwa mujibu wa mkataba huu, mdhamini/wadhamini watawajibika wakati wowote kumhimiza mkopaji kulipa deni lake na kwamba ikitokea mkopaji ameshindwa kulipa deni lake hatua za kisheria zilizotajwa katika sharti la 13 na 14 hapo juu zitachukuliwa dhidi ya mdhamini au msimamizi wa mirathi ya mdhamini.
16. Mkopaji anakubali taarifa zilizotolewa ndani ya mkataba huu zitutmike katika usimamizi wa mikopo.
17. Mkataba huu hautaathiri masharti mengine ya lazima kuhusu mikopo yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria za **HAI RURAL TEACHERS SACCOS LTD**, Masharti au Sera ya mikopo ya **HAI RURAL TEACHERS SACCOS LTD.**
18. Sheria za Ushirika za Tanzania na Sheria ya Huduma Ndogo za Kifedha pamoja na Kanuni zake zitatumika kutatua suala au mgogoro wowote kuhusu mkataba huu.
19. Fomu ya mkopo na fomu nyingine zitakazosainiwa na mkopaji zitakuwa sehemu ya mkataba huu.

**KWA KUZINGATIA USHUHUDA ULIOTOLEWA MKATABA HUU UMESAINIWA NA WAHUSIKA SIKU, TAREHE, MWEZI NA MWAKA KAMA IFUATAVYO**

…………………………………………………… *(jina la mkopaji)* ambaye
anaelewa lugha iliyotumika katika uandaaji
wa mkataba huu leo tarehe…….. mwezi………mwaka …………..

………………………
**Sahihi ya Mkopaji**

………………………………………………..*(taja jina la afisa )* ambaye
anaelewa lugha iliyotumika katika uandaaji
wa mkataba huu leo tarehe …….. mwezi………mwaka…....…

……...……………….
**Sahihi na muhuri wa Mkopeshaji**
(mwakilishi wa mkopeshaji)

***MBELE YA: WAKILI/HAKIMU***

***JINA…………………………….................................***

***SAINI…………………………………………***

***MUHURI……………………………………………***

***TAREHE…………..........................***